# USALAMA BARABARANI

**Set song**

# 28/08/2015

*Wiki ya nenda kwa Usalama.*


Na. Sambaya Edmund C.
Bunazi sec.&High school.
S.L.P 79.
Kyaka-Missenyi
BUKOBA-TANZANIA.
CALL; 0759564088/0655640888/0783868791.


**Friday**




# KIITIKIO







**3.Magari ya safari ndefu, Mabasi na hayo malori,**
**Zingatieni na sheria, Ajali msisababishe,**
**Udereva wa kujihami, Siku zote zingatieni,**
**Ti sheria bila shuruti, Okoa Maisha dereva.**

**5.Nawe mwendesha pikipiki, Sheria nazo zingatia,**
**Kofia ngumu uivae, Wewe na abiri wako,**
**Kamwe usije kupakiza, Abiria wengi dereva,**
**Heshimu pia vivuko, Vya watembea kwa miguu.**




**4.Madereva muendeshapo, tahadhari zingatieni,**
**Uegeshaji wa magari, barabarani zingatia,**
**Waendeshaji baiskeli, mikokoteni maguta,**
**Endesha chombo kwa salama, uweze okoa maisha.**

**6.Na elimu ya udereva ni muhimu kuipata,**
**Utaendesha chombo chako, kwa kuzifuata sheria,**
**Abiria katika chombo, kemea vitendo viovu,**
**Pia utoe taarifa, kwa askari aulizapo.**

***Ajali za barabarani jamani***
***wapendwa zimekuwa kilio***
***cha wana familia, wanajamii,***
***na taifa kwa ujumla kwani***
***Tumewapoteza ndugu zetu wengi,***
***Hasa vijana ambao***
***wengi wetu ni waendesha***
***pikipiki maarufu kwa jina la***
***BODABODA, Waendesha***
***magari wakiwa walevi na***
***wengine kutojali sheria za***
***barabarani na kusababisha***
***ajali na kuwaua abiria wengi***
***na hata wengine kujeruhiwa vibaya,***
***Ee Mungu wapumzishe***
***Marehemu wote wa ajali***
***barabarani na wengine wote***
***Mahali pema milele mbinguni. AMINA.***